



Hakika mtu mwenye adhabu nafuu katika watu wa motoni ni yule atakayekuwa na viatu viwili na soli mbili vitokanavyo na moto, utakuwa ukitokota kwa hivyo ubongo wake kama kinavyotokota chungu, hatona kuwa kuna yeyote mwenye adhabu kali kuliko yeye, kumbe yeye ndiye ana adhabu nafuu kuliko wote

kutoka kwa Nu'man bin Bashiri -radhi za Allah ziwe juu yake- amesema: Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu -rehema na amani ziwe juu yake-: "Hakika mtu mwenye adhabu nafuu katika watu wa motoni ni yule atakayekuwa na viatu viwili na soli mbili vitokanavyo na moto, utakuwa ukitokota kwa hivyo ubongo wake kama kinavyotokota chungu, hatona kuwa kuna yeyote mwenye adhabu kali kuliko yeye, kumbe yeye ndiye ana adhabu nafuu kuliko wote"

[Sahih] [Wamekubaliana Bukhaariy na Muslim]

Ameeleza Mtume rehema na amani ziwe juu yake kuwa mtu mwenye adhabu nafuu katika watu wa motoni siku ya Kiyama ni yule atayekuwa na viatu viwili na soli mbili, utakuwa ukichemka ubongo wake kutokana na kuchemka kwake, kama linavyochemka sufuria la shaba, na wala hatona kuwa kuna yeyote mwenye adhabu kali zaidi yake, kumbe yeye ndiye mwenye adhabu nafuu zaidi kuliko wote, na hii ni kwa sababu zitakusanyika kwake adhabu zote mbili, adhabu ya mwili na adhabu ya nafsi.

<https://sunnah.global/hadeeth/sw/show/4220>

